

## **Umbuji wa Watani katika Maombolezo ya Wangoni: Uchunguzi wa Vipengele Teule vya Fasihi**

*Martina Duwe*<sup>1</sup>

### **Ikisiri**

Kiasili, Wangoni hutumia utani kama nguzo muhimu ya kufikisha maudhui lengwa kwa hadhira, hususani katika shughuli mbalimbali za kitanzia na kiramsa. Katika shughuli za kitanzia, mathalani, maombolezo; watani hutumia umbuji unaozingatia kaida zao ili kufikisha ujumbe fulani kwa hadhira husika. Umbuji huo huweza kubainika kupitia sanaa za maonesho, kama vile uchezaji wa ngoma na matumizi ya lugha ya kibunifu inayoambatana na vitendo mbalimbali kama uigizaji na uimbaji. Hata hivyo, haijawa bayana ni kwa namna gani uwasilishaji wa maudhui hayo kupitia vipera vya fasihi simulizi unabainisha umbuji unaosawiri maisha yao halisi. Kwa hiyo, makala hii inafafanua jambo hilo kwa kurejelea maombolezo ya jamii ya Wangoni. Haya ni matokeo ya utafiti uliofanyika katika mazingira halisi ya Wangoni. Data za utafiti huu zilipatikana kwa mbinu za ushuhudiaji katika matukio yanayoambatana na suala la mazishi pamoja na usaili. Vilevile, misingi ya Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi imetumika kama mwegamo mkuu katika kuchunguza, kuchambua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Matokeo yanaonesha kuwa watani katika maombolezo ya Wangoni wana dhima kubwa ya kufikisha maudhui kwa jamii kupitia umbuji unaosawiri utamaduni wao. Hivyo, makala hii inajadili umbuji huo kwa kujiegemeza katika vipengele teule vya fasihi simulizi ambavyo ni: maigizo, nyimbo na semi.

### **1.0 Utangulizi**

Fasihi simulizi ni nguzo muhimu katika maombolezo ya jamii nyingi za Waafrika. Maombolezo kwa Waafrika huhusisha maneno ya huzuni au masikitiko yanayosemwa au kuimbwa na watu au mtu anayefikwa na tatizo, hususani msiba (Khosha-Nkatini, 2022). Kila jamii ina namna yake ya kuomboleza ikiwa na madhumuni ya kuwafariji wafiwa, kuonesha hisia za jamii na kuendeleza misingi ya ushirikiano miongoni mwao. Migodela (2019) anaeleza kwamba kuomboleza kunasaidia kuondoa uchungu na maumivu ya ndani yanayomkabili mtu. Kimsingi, katika maombolezo hayo, maudhui yanayoisawiri jamii husika huwasilishwa. Namna ya kufikisha maudhui kwa hadhira lengwa hukitwa katika misingi

---

<sup>1</sup> Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania. Barua pepe: [magriccola@gmail.com](mailto:magriccola@gmail.com)

inayozingatiwa na jamii husika (Miruka, 2005). Kwa Wangoni, maombolezo ni mchakato unaoanza mara tu baada ya kutokea kwa tatizo. Kimahususi katika mazishi, maombolezo yanaweza kumulikwa katika namna kuu mbili. Kwanza, maombolezo yanayofanyika wakati wa mazishi ambayo hujumuisha jamii nzima na hutoa fursa kwa watani kuwasilisha maudhui lengwa kwa hadhira kulingana na taratibu na mipaka yao ya kutaniana. Vitendo vya watani katika maombolezo hayo ndivyo vilivyotafitiwa na kujadiliwa katika makala hii. Pili, maombolezo ya baada ya mazishi ambayo huhusisha zaidi familia na hufanyika kwa kipindi fulani kulingana na kaida zao, mathalani, miezi sita au mwaka mmoja.

Utani ni utaratibu wa kimila ambao unaruhusu jamii fulani za watu kuelezana au kutendeanana mambo yoyote bila kukasirikiana (Mzandi, 2011). Utani katika jamii za Kiafrika hukuza ushirikiano na uhusiano baina ya kabila, koo na familia, ambapo mtu huweza kutamka neno lolote lenye funzo fulani au kuchukua vitu vya mtani wake bila kuleta athari yoyote miongoni mwao. Katika misiba, utani una dhima mbalimbali kama vile kuwaliwaza wafiwa, kurekebisha mienendo ya jamii na kuendeleza utamaduni wa jamii (Mlaga, 2017; Kutwa, 2021). Kwa mantiki hiyo, utani ni mchakato wa kitamaduni unaoruhusu jamii au watu fulani kutaniana. Utani haufanywi kiholela, bali huzingatia taratibu, masharti na mipaka ya kiumri, nafasi, uhusiano na hali za wanaotaniana. Katika maisha ya Wangoni, utani hutumika kama nyenzo muhimu katika kufariji, kukosoa, na kuelimisha jamii. Watani hao hutumia umbuji unaokidhi misingi ya kaida zao katika kuwasilisha maudhui kwa hadhira lengwa.

Umbuji ni dhana inayorejelea wasifu wa kazi ya kifasihi unaohusisha sifa za kiufundi na upekee wa kueleza au kuwasilisha maudhui fulani (Wamitila, 2003). Kila jamii inatumia ufundi unaozingatia sanaa inayosawiri maisha yao halisi. Aghalabu ufundi unaotumika katika kufikisha maudhui lengwa kwa hadhira ndio unaobainisha na kuitofautisha kazi moja ya sanaa na nyingine. Kirumbi (1975) na Okpewho (1992) wanaeleza kwamba katika fasihi ya Waafrika, ufundi wa kuwasilisha maudhui kwa hadhira lengwa hujikita katika kanuni za maisha za jamii husika ambazo zinaweza kuwa na utofauti fulani na jamii nyingine. Ufundi huo hutegemeana na misingi ya mila na desturi za jamii katika uzingatizi wa lugha, vitendo na wakati unaohifadhi na kulinda falsafa na historia ya fasihi ya jamii husika (M'Ngaruthi, 2008; Mulokozi, 2017). Watani hutumia umbuji unaosawiri utamaduni wa jamii yao ili kufikisha ujumbe husika. Kwa kuzingatia hilo, makala hii inajadili umbuji wa watani wanaopatikana katika jamii ya Wangoni waishio nchini Tanzania pekee ili kuonesha ufundi wa ufikishaji wa maudhui yao kwa hadhira lengwa wakati wa maombolezo kwa kumakinikia vipengele teule vya kifasihi.

Wangoni ni jamii pana inayopatikana nchini Tanzania, Malawi, Msumbiji, Kongo na Zambia. Historia inaonesha kwamba asili ya kabila hili ni nchi ya Afrika ya Kusini, hususani katika eneo la Kwa Zulu-Natal (TIE, 2019). Nchini Tanzania, Wangoni ni jamii mojawapo inayopatikana kusini mwa nchi hiyo, hususani katika

mkoa wa Ruvuma. Kabila hili hutofautiana na jamii nyingine kutokana na sifa zake mahususi za kiutamaduni, kijamii na kiuchumi. Kabila hili hujumuisha jamii ndogondogo tatu ambazo ni: Wamatengo, Wandendeule na Wangoni (Ngonyani, 1988; Ebner, 2009). Katika kuishi kwao, Wangoni hujifungamanisha na masuala mbalimbali yanayodhihirisha ustawi wao kama jamii mojawapo iliyopo Tanzania. Miongoni mwa masuala hayo ni namna ya uombolezaji wao unaokwenda sambamba na uzingatizi wa mila na desturi zao ambapo fasihi simulizi hutumika kama kijenzi muhimu katika kuwasilisha maudhui kwa hadhira inayokusudiwa.

Kwa sasa, imebainika kuwa umbuji wa watani katika uwasilishaji wa maudhui hayo wakati wa maombolezo hukitwa katika matumizi ya lugha kuu mbili ambazo ni Kingoni na Kiswahili. Hata hivyo, matumizi ya lugha hizi mbili, hayaathiri ufikishaji wa maudhui husika kwa hadhira kupitia fasihi simulizi inayotumiwa na watani wao. Sambamba na hayo, katika maombolezo yao, lugha hizi hutumika kwa ustadi unaokidhi misingi ya utamaduni wao. Imebainika kuwa hakuna ulinganifu wa uchopekaji wa vionjo mbalimbali vya lugha ya Kingoni au Kiswahili wakati wa uimbaji, uigizaji na utoaji wa semi zao. Vionjo hupachikwa kutegemeana na mazingira ya msiba husika na umahiri wa watani kwa kuzingatia maudhui yanayolengwa kuwasilishwa kwa wakati husika (Duwe, 2022). Kwa hiyo, makala hii inafafanua namna watani wanavyotumia umbuji wao katika kuwasilisha maudhui hayo kwa kujiegemeza katika lugha zote mbili, yaani Kingoni na zenye mchanganyiko wa lugha ya Kingoni na Kiswahili. Aidha, data zilizowasilishwa kwa lugha ya Kingoni zimetolewa fasiri ili kukidhi matakwa ya lugha asili ya makala hii ambayo ni Kiswahili.

## **2.0 Mwegamo wa Nadharia**

Makala hii ni matokeo wa utafiti uliofanyika kwa kujiegemeza katika misingi ya Nadharia ya Kisosholojia ya Kifasihi. Coser (1963) anaeleza kwamba nadharia hii iliasisiwa na Charles Taylor (1822-1917) pamoja na George Lukacs (1885-1971). Wataalamu hawa wanaimulika kazi ya fasihi kama zao la kijiografia, kiutamaduni na mazingira ya jamii husika. Kwa mantiki hiyo, kazi ya sanaa, hasa fasihi inatakiwa iakisi taarifa za kweli kuhusu maisha halisi ya jamii. Kimsingi, nadharia hii hujikita katika kumulika na kubainisha uhusiano uliopo baina ya kazi ya kifasihi na jamii iliyoiunda kazi hiyo. Zaidi ya hayo, nadharia hii hufafanua sababu za kutokea, kuibuka, na kutendeka kwa kazi ya fasihi yenye umbo la kijamii na namna mtazamo wa msanii wa kazi hiyo unavyoongozwa na mila, desturi na maisha halisi ya jamii husika. Kwa ujumla, msisitizo wa nadharia hii upo katika kutazama namna kazi ya fasihi inavyohusiana na maisha halisi ya jamii husika. Naye Glicksberg (1972) anaeleza kwamba fasihi na mazingira ya jamii husika haviwezi kutenganishwa. Hivyo, katika uhakiki wa kazi za kifasihi ni vyema uhusiano wa vipengele vyake, yaani fani na maudhui ulandane na mazingira halisi ya jamii. Jambo hili limezingatiwa katika utafiti ulioleta matokeo haya ambapo nadharia hii imekuwa mwegamo mkuu katika kuchunguza, kuchanganua na

kuwasilisha data zinazohusu namna maudhui yanavyowasilishwa kwa kujiegemeza katika maigizo, mbolezi na semi zitolewazo na watani katika maombolezo ya Wangoni.

### **3.0 Methodolojia**

Mchakato mzima wa uchunguzi na uchakataji wa matokeo ya makala hii umejiegemeza katika mkabala wa kitaamuli. Data zilikusanywa uwandani, mahususi katika mkoa wa Ruvuma, Halmashauri ya Songea Vijijini ambapo vijiji vinne kutoka kata mbili za Maposeni na Kilagano vilihusishwa. Vijiji hivyo ni Lugagara, Mdunduwalo, Mgazini na Maposeni. Mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data za matokeo haya ni mbili, nazo ni ushuhudiaji na usaili. Mtafiti alishuhudia matukio mbalimbali katika mazishi ya vifo nane ili kupata data za matokeo haya. Ushuhudiaji huo ulilenga kuchunguza vitendo vya kifasihi vilivyofanywa na watani ambapo katika andiko hili vimebainishwa kwa herufi X1 hadi X5. Katika usaili, watani wanane wanaohusishwa katika shughuli zinazoambatana na kifo walishiriki katika mchakato wa upatikanaji wa data za matokeo haya. Kutokana na uzoefu na umilisi wao wa mila na desturi za jamii hiyo, hawa waliteuliwa kama sampuli ya kuwakilisha watani wengine wenye sifa hiyo. Watani hawa walipatikana kwa mbinu ya usampulishaji lengwa tajwa. Katika makala hii wamebainishwa kwa herufi A hadi H.

### **4.0 Umbuji wa Watani katika Maombolezo ya Wangoni**

Matokeo yanaonesha kuwa upatikanaji wa watani katika jamii ya Wangoni ni suala linalotokana na mambo ya kiutamaduni na kihistoria. Kuna watani wa namna kuu mbili ambao ni: kwanza, wale wa ndani ya jamii, yaani koo fulani kutoka kwa Wangoni wenzao. Kwa hiyo, sio kila ukoo unaruhusiwa kufanya utani na ukoo fulani. Pili, utani wa nje ya jamii yao, yaani kabila tofauti kama vile Wahehe na Wabena wanaoishi katika eneo lao. Imebainika kuwa kila kundi lina mipaka yake katika kutenda shughuli fulani wakati wa maombolezo. Mathalani, watani kutoka nje ya jamii yao huishia kufanya shughuli zisizohusisha kiwango cha juu cha uzingatizi wa tamaduni za jamii hiyo. Hivyo, mara nyingi hushiriki katika kuwasilisha maudhui kwa hadhira kwa kuimba, kuchekesha na kuigiza wakishirikiana na watani wa ndani. Aidha, shughuli kama vile kuandaa mwili wa marehemu na kukamilisha shughuli fulani za mazishi, mathalani, kuwaoggesha na kuwanyoa wafiwa hufanywa na watani wa ndani ya jamii pekee. Hii ni kutokana na umilisi wa uzingatizi wa tamaduni zao katika kufanya shughuli hizo. Pamoja na hayo, watani kutoka ndani ya jamii ndio wamebainika kuwa na mchango mkubwa katika kutenda na kuwasilisha maudhui lengwa kwa hadhira kwa kutumia umbuji unaokidhi misingi ya utamaduni wao. Hivyo, katika makala hii tunabainisha umbuji huo kupitia semi, maigizo na mbolezi.

#### 4.1 Semi

Semi ni kauli fupi ya kisanaa yenye kubeba maana, mafunzo au ujumbe fulani kwa jamii kama vile: methali, nahau, mafumbo, vitendawili, lakabu, mizungu na misemo (Mlaga, 2017). Utanzu huu huweza kutumika wenyewe kama kifungu kilichokamilika katika kufikisha ujumbe unaolengwa. Hata hivyo, katika utendekaji wa tanzu nyingine za fasihi, mathalani, maigizo na ushairi, utanzu wa semi huweza kuchopakwa ili kukamilisha vyema mtiririko wa ufikishaji wa maudhui lengwa kwa hadhira (Simiyu, 2015). Kwa msingi huo, tanzu za semi zina mchango mkubwa katika kujenga mtiririko wa tanzu nyingine za fasihi simulizi. Matokeo yanaonesha kwamba katika maombolezo ya Wangoni watani hutumia semi zinazosawiri kaida za jamii hiyo. Semi, mathalani, za kejeli, kusifu au kuonya, hutumika kulingana na ulazima wa ufikishaji wa maudhui fulani kwa hadhira husika. Hili hufanyika kutegemeana na maamuzi pamoja na ujuzi wa mtani. Imebainika kuwa semi zitumiwazo zaidi na watani katika maombolezo yao ni misemo na mafumbo.

Tukianza na misemo, hii ni semi fupi isiyohitaji jibu la papo kwa hapo ila maana yake hutokana na tafakuri kulingana na misingi ya tamaduni za jamii husika (Mauya, 2006). Katika maombolezo ya Wangoni, misemo huweza kubainika katika kifungu cha semi chenye kuwasilisha maudhui lengwa. Kifuatacho ni kifungu cha semi kilichosheheni misemo mbalimbali ya Kingoni na kinawasilishwa na mtani XI.

*Mwenga lelu mlolayi mang'ova<sup>2</sup>. Mau winu ahekeye na vandu, mwavana nyenye mwimeka pa mlima apa. Mtamayi mwakamanyayi mlima uwu tawoha tukuuleka. Eti, mwitama nu nyumba ya mbwina, eti nyina winu akavili na mene, ng`uku na migunda. Hinu muvili nu nu, mchikolili lelu. Mhekayi na vandu mwenga. Mwilola pahi lelu, chivavina?" Mwilola lelu nu mau avililepi panyumba apa. Mlolayi ga vayinu mwenga. Mkotokai kulola pahi apa, mlolali na kunani mwenga.*

Jamani leo muone ukiwa mahali hapa. Mama yenu alikuwa mtu wa watu, nyie watoto mnaringa hapa duniani. Mkae mkijua dunia hii sote tutaiacha. Mnakaa kimya kwa vile mna nyumba nzuri, mama yenu ana mbuzi, kuku na mashamba. Sasa mpo kimya, mmeipata jeuri yenu. Mcheke na watu jamani. Mnatazama chini leo, panawauma? Leo kimya mama hayupo tena hapa nyumbani. Mtazame kwa wenzio. Msitazame hapa chini pekee, mtazame juu pia (Tafsiri ya Mtafiti).

**Chanzo:** Utafiti (2023)

---

<sup>2</sup> Maana yake katika lugha ya Kiswahili ni makazi yaliyoachwa baada ya mtu kuhama au kufariki. Mara nyingi makazi haya yanakosa mtunzaji, kwa hiyo, kuonekana yamechakaa au hayafai kukaliwa. Dhana hii hutumika kuonesha pengo la aliyeondoka kwa waliobaki.

Nukuu hiyo imetawaliwa na misemo inayotumiwa na watani katika kuwasilisha maudhui yanayohusiana na suala la kifo. Matokeo yanaonesha kuwa wakati mtani anayasema haya, huketi jirani na wafiwa na huonesha vitu vinavyomzunguka huku akicheka kuonesha hisia za shangwe katika kufikisha maudhui yake. Kupitia nukuu hii tunabaini kuwa kuna semi zinazozingatiwa katika jamii hiyo. Kwa mfano, *mlolayi ga vayinu* ni msemu unaolenga kuwahimiza watoto na ndugu wa marehemu kushiriki katika matatizo ya wengine. Imebainika kuwa watani wanapowasilisha maudhui yao kupitia misemo, nyuso zao huonesha hisia za shangwe zenye kuwakejeli wafiwa. Haya yanabainishwa zaidi na msailiwa A anayesema: “Tunapotaka kufikisha ujumbe kwa walengwa tunavaa nyuso za kazi. Hakuna aibu wala kupepesa macho. Tunafurahi huku tukiwakejeli na kuwaeleza ukweli ili wabadilike. Tunaweza kutumia misemo ya kuwaumiza huku tukicheka na kuonesha tabasamu kwa wafiwa”. Matokeo yanaonesha kuwa *mhekayi na vandu* kama inavyobainika katika kifungu cha semi hapo juu ni msemu unaotumika katika jamii hiyo ili kutoa funzo kwa wasiopenda kushiriki shughuli za kijamii, hasa mazishi. Sambamba na hayo, msemu *lelu muvili nu nu* hutamkwa kwa ufundi mkubwa unaoambatana na kejeli inayobainika katika sura ya mtamkaji. Vilevile, sauti na madoido ya utamkaji wa msemu huu huleta tafakuri kwa wafiwa kwamba hawana la kufanya ila kutegemea msaada wa jirani na jamii kwa ujumla. Imebainika kwamba misemo hiyo katika maombolezo ya Wangoni, aghalabu huwasilishwa kwa lugha ya kejeli. Matumizi ya kejeli husawiri maisha halisi ya Waafrika kama asemavyo Mrikaria (2010) kwamba jamii ya Waswahili kama sampuli mojawapo ya Waafrika, hutumia kejeli inayosawiri utamaduni wao katika kufikisha ujumbe unaokusudiwa.

Pamoja na misemo hiyo, umbuji wa watani katika maombolezo ya Wangoni hubainika kupitia mafumbo yanayotumika katika jamii yao. Mafumbo ni semi fupi ambazo maana zake zimefichika kabisa na huhitaji jibu la papo kwa hapo (Simiyu, 2011). Matokeo yanaonesha kwamba kwa Wangoni, mara nyingi kipera hiki cha semi huweza kuambatana na aina nyingine ya semi kama vile misemo. Kwa mfano, katika nukuu hiyo ya awali, semi isemayo *mwilola pahi lelu, chivavina? yenye* maana ya ‘mnatazama chini leo, kinawauma?’ ni fumbo linalohitaji jibu kutoka kwa wafiwa. Mtani anapotamka maneno haya hutazama nyuso za wahusika na sauti yake huwa kali ikiashiria kutaka kusikia au kuona mwitiko wa namna fulani kutoka kwa walengwa. Imebainika kuwa inapotokea fumbo limetolewa wafiwa hutoa jibu ili kuomba msamaha. Kwa mfano, huweza kusema *pepayi, tibudili tete* ikiwa na maana ya ‘tafadhali, tumekosa’. Matokeo yanaonesha kwamba si lazima watamke wote. Anaweza akatamka mmoja au mtani mwingine kwa niaba ya wahusika wengine. Vilevile, anaweza asitoe sauti katika kuomba msamaha huo bali akapiga magoti mbele ya mtani na kushika miguu yake kwa unyenyekevu kuashiria kwamba wao ni wakoaji, hivyo, wanahitaji kusamehewa. Kushadidia hili, ilishuhudiwa mtani X2 anapiga magoti mbele ya mtani aliyetoa mafumbo kwa niaba ya wafiwa. Kitendo hiki kinakwenda

sambamba na uitikiaji au kukubaliana na yanayoelezwa na mtani huyo kwa kutumia viungo mbalimbali vya mwili wake, ikiwamo mikono na kichwa.

Utambuzi wa maana za umbuji wa watani kupitia mafumbo yao huhitaji umilisi wa tamaduni za jamii hiyo. Kwa msingi huo, kwa mtu ambaye hana uzoefu wa maisha ya jamii hiyo hawezi kuwa na ufahamu juu ya maana za mafumbo hayo kama anavyoeleza Mulokozi (2017) kuwa mafumbo humtaka anayeulizwa atumie akili na udadisi ili kupata maana iliyokusudiwa na fanani. Udadisi huo hutokana na umilisi wa tamaduni za jamii husika. Kimsingi, mjadala huu unaonesha kuwa hakuna fomula ya kuwasilisha maudhui lengwa kupitia mafumbo yao. Haya yanafafanuliwa zaidi na msailiwa B anaposema:

Kuna familia nyingine inajiona kama itaishi duniani milele. Haishiriki kwa wenzao, hasa panapotokea kifo. Kwa hiyo, lazima sisi watani tuwaonye na kuwaasa kwamba kuishi ni kushirikiana na wengine, hasa wakati wa shida. Kwa mantiki hiyo, tunaongea kwa mafumbo na kutumia misemo mbalimbali kulingana na ujumbe tunaohitaji kuufikisha kwao. Familia yenye kuishi kwa kuzingatia tamaduni zetu hatuongeiongei ovyo. Tunafanya yale ya msingi tu na kushirikiana nao vema katika kuomboleza. Kwa jumla, watani katika jamii hii tuna nguvu sana katika kubadilisha tabia za watu, hasa panapotokea kifo. Ujumbe unaotolewa na mtani si kwamba ni kwa ajili ya wafiwa pekee, bali huwalenga watu wote ndiyo sababu hatuwanong'onezi, bali tunaongea kwa sauti ili jamii nzima isikie na kujitafakari.

**Chanzo:** Utafiti (2023)

Nukuu hii inathibitisha wazi kwamba watani hutumia semi ili kutoa mafunzo fulani kwa hadhira kulingana na ulazima wa kufanya hivyo. Kwa kuongozwa na mtazamo wa wanasosholojia kuwa fasihi na maisha halisi ya jamii haviwezi kutenganishwa, semi za Wangoni huakisi misingi ya utamaduni wa jamii hiyo. Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kwamba wakati wa uwasilishaji wa maudhui kupitia semi, mtani haweza kuketi au kusimama jirani na wafiwa na kupaza sauti yake. Wakati mwingine huwaomba waombolezaji wengine wakae kimya ili apate nafasi ya kuwasilisha vyema maudhui lengwa. Hufanya hivyo kwa kuwa anaamini kwamba ujumbe unaolengwa kuwasilishwa hupaswa kufika kwa hadhira yote ili kila mmoja atafakari kiwango cha ushiriki wake katika masuala ya kitanzia. Vilevile, anakusudia kuujulisha umma kuwa familia iliyopatwa na msiba haina ushirikiano ambapo ni kinyume na matakwa ya jamii kwa ujumla. Kwa hiyo, wabadilike na watazamwe kwa upya katika misiba mingine itakayotokea kijijini hapo kama wahenga wasemavyo *umoja ni nguvu utengano ni udhaifu*. Haya yanafafanuliwa na msailiwa C kama alivyoeleza: “Mtani anapokabidhiwa jukumu anakuwa na dhamana ya kuiwakilisha jamii. Wakati mwingine, watu wakijua wewe ni mtani katika msiba huo wanakudokeza hisia zao ili uone namna ya kuziwasilisha. Tunalikamilisha hilo kwa kutumia ufundi mkubwa kama vile lugha

ya mafumbo na misemo pasipo kuathiri ukweli wa maana inayokusudiwa”. Hivyo, watani katika maombolezo husikilizwa kutokana na umuhimu wao kama asemavyo Mzandi (2011) kwamba watani katika misiba ya Waafrika hupewa thamani kwa kuwa wana dhima ya kurekebisha mienendo ya jamii, kuhifadhi na kuendeleza mila na desturi za jamii.

#### 4.2 Maigizo

Umbuji wa watani katika maombolezo ya Wangoni hubainika pia kupitia uigizaji unaofanyika mbele ya hadhira. Maigizo ni sanaa ya utendaji yenye kuhusisha lugha ya kibunifu na vitendo vinavyosawiri utamaduni halisi wa jamii na hufanyika kwa madhumuni ya kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira lengwa (Okpewho, 1992). Vitendo mbalimbali huhusishwa wakati wa utendakaji wa maigizo hayo kama vile kuchekesha, kujigamba na kulumbana au kujibizana baina ya pande mbili. Uigaji wa vitendo hivyo hutegemeana na azma ya maudhui yanayowasilishwa. Kwa minajili hiyo, katika sanaa za maonesho za jamii nyingi za Kiafrika, vitendo ikiwamo uigaji hufanyika kulingana na haja ya kuwasilisha ujumbe fulani (Miruka, 2005). Kwa hiyo, hakuna namna moja ya kuigiza katika shughuli mbalimbali za kijamii, hususani mazishi. Anaeleza kwamba katika baadhi ya makabila, maigizo ya misibani hufanywa na watani au wajukuu wa marehemu. Ndivyo ilivyobainika katika misiba ya Wangoni kwamba watani ndio wenye jukumu la kuigiza wakati wa maombolezo yao. Maigizo hayo hudhihirika bayana kupitia vichekesho na malumbano baina ya pande mbili.

Kwa kuanza na vichekesho, matokeo yanaonesha kuwa watani katika maombolezo ya Wangoni hutumia mbinu ya uchekekeshaji unaosawiri utamaduni wao katika kufikisha maudhui yanayokusudiwa. Imebaika kwamba mtani mmoja anaweza kuchekesha kwa sauti kubwa mbele ya hadhira baada au kabla ya maziko. Madhumuni ya kutumia sanaa ya uchekekeshaji katika maombolezo ya Wangoni ni kuonya na kukemea tabia zisizofaa katika jamii hiyo kwa namna isiyowahuzunisha walengwa. Hivyo, hadhira hupata ujumbe husika huku nyuso zao zikiwa na furaha. Zaidi, ilishuhudiwa mtani X3 akitoa kichekesho mbele ya hadhira kuhusu mwenendo wa marehemu na familia yake kwa ujumla. Hapa anawasilisha:

(Mtani akivuta kiti na kuvaa koti lake. Kisha anaketi huku akikunja nne) *Mwenga mwenga!* (watu wote kimya) *lelu vapatikini mwenga* (anasimama na kuweka kijiti mdomoni) *vyajova vifwa lepi. Mwenga pamlima apa lelu gavili koki?* (anaketi). (Anaigiza sauti ya marehemu) Mimi kila jioni lazima nipumzike hapa. Mama Jeni *letayi muyakaya wangu uvili muchijomela chivaa chila. Kitayi nyata wenga. Ahaa! Kumalilu nihamba chilau. Lelu ninywa hoti muyakaya ululili kweli. Mwenga muyakaya uwu kunyambaaa!* (ananyanyua chombo chenye pombe ile na kunywa taratibu)

(Mtani akivuta kiti na kuvaa koti lake. Kisha anaketi kwenye kiti huku akikunja nne). Jamani, jamani! (watu wote kimya) leo wamepatikana



jamani (anasimama na kuweka kijiti mdomoni) walijua hawafi. Jamani hapa duniani leo yako wapi? (anaketi). (Anaigiza sauti ya marehemu) Mimi kila jioni lazima nipumzike hapa. Mama Jeni lete hiyo pombe ipo kwenye kisonjo kikubwa hicho. Ufanye upesi. Ahaa! Msibani nitakwenda kesho. Leo nakunywa kwanza hii pombe nzuri sana. Jamani pombe hii ina ubora sana! (ananyanyua chombo chenye pombe na kunywa taratibu - Tafsiri ya Mtafiti).

**Chanzo:** Utafiti (2023)

Kichekesho hicho kinabainisha hisia za jamii kuhusu mwenendo wa wafiwa juu ya kutoshiriki katika misiba inayotokea katika eneo lao. Wakati wa uwasilishaji wa maudhui, mtani anavaa uhusika wa marehemu na huchekesha huku akifanya vitendo ambavyo alivishuhudia vikifanywa na marehemu wakati wa uhai wake. Hapa anafanya vitendo kama vile, kuvaa koti, kusimama, kuketi juu ya kiti au mkeka, kuweka kijiti mdomoni ikiwa ni ishara ya kuvuta sigara na kunywa pombe. Vilevile, imebainika kuwa mtani anaweza kutumia vitu halisi na (au) visivyo halisi katika uchekekeshaji wake. Matendo haya yanaikumbusha jamii kuhusu tabia na mwenendo wa marehemu wakati wa uhai wake. Pia, imebainika kuwa mtani huiga sauti ya marehemu na kutamka maneno kiubunifu kama alivyokuwa akiyatamka. Umbuji huo wa kuwasilisha maudhui huifanya hadhira ifurahi huku ikitafakari ujumbe unaowasilishwa kama asemavyo msailiwa D: “Tunatoa ujumbe kwa njia ya furaha ili hadhira isichoke kusikiliza. Mtani ana uwezo wa kubainisha tabia halisi za familia kwa njia ya kufurahisha”. Kimsingi, ujumbe katika kichekesho hiki unaleta tafakuri kwa wafiwa na jamii kwa ujumla kwamba kutoshiriki katika misiba ni jambo lisilopendezwa na jamii nzima, hivyo, kila mmoja anapaswa kubadilika. Kwa mantiki hiyo, fasihi ni akisio la yale yanayotokea katika jamii kama inavyoelezwa na wanasosholojia kuwa huwezi kuitenganisha fasihi na mazingira halisi ya jamii. Umbuji unaotumiwa na watani katika kuwasilisha maudhui huakisi utamaduni wa jamii hiyo. Kwa ujumla, uwasilishaji wa maudhui haya kupitia vichekesho vyao huzingatia ukweli wa maisha ya wafiwa katika jamii yao. Sambamba na nukuu hiyo ya kichekesho, msailiwa E anashadidia hili kwa kusema:

Wangoni kuchekesha jamii ni jadi yetu. Mara nyingi tunatumia vichekesho katika kufikisha ujumbe fulani kwa jamii. Si tu katika masuala ya furaha, hata msibani uchekekeshaji hufanyika ila kuna mipaka yake ambapo si kila mtu ana jukumu la kufanya hivyo. Ukiwa mtani na una uwezo wa kuchekesha unaruhusiwa kufanya hivyo. Kiuhalisi, hakuna anayependa kufiwa ambapo katika jamii yetu tunalichukulia jambo hilo kwa uzito wa pekee sana. Hata hivyo, kuna wasiojali wala kuthamini kuwa shughuli za mazishi zinapaswa kufanywa na watu wote. Wakati wa maombolezo tunachekesha ili kuwaonya na kuwataka wabadilike. Mara nyingi uchekekeshaji hufanyika wakati wa maombolezo katika familia isiyoonsha

ushirikiano kwa wengine. Uchekeshaji huo hubeba taswira ya masimango yanayoakisi utamaduni wetu. Vilevile, watani pamoja na majukumu yetu mengine, tunatoa ujumbe kwa jamii nzima kwa jumla. Hii yote ni kuikumbusha jamii kuwa kila mmoja anapaswa kuwajibika vema katika shughuli za mazishi hapa kijijini. Kwa jumla, lugha ya kejeli tunaiona kuwa nzuri kuitumia wakati wa kuchekesha kwa kuwa inawafanya wahusika watafakari kwa kina kutokana na ujumbe waliousikia.

**Chanzo:** Utafiti (2023)

Maelezo haya yanaonesha kwamba umbuji unaotumiwa na watani katika kuwasilisha maudhui lengwa kwa jamii unaweza kuleta burudani fulani inayosababisha kuibuka kwa hisia za furaha miongoni mwao. Kadhalika, mwonekano na vitendo halisi vinavyofanywa na mtani huakisi sifa za uchekeshaji ambapo huleta msisimko kwa watazamaji wakati wa maombolezo. Kwa mfano, anaweza kupaka jivu usoni, kuvaa miwani yenye jicho moja bovu, kuvaa shati au suruali iliyochakaa, kupiga na kutumia miondoko ya madaha. Hata hivyo, umbuji huo hauathiri azma yake ya kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Matokeo yanaonesha kuwa maudhui ya msingi katika uchekeshaji huo hulenga kuikosoa na kuionya jamii kuhusu tabia ya kutoshiriki katika shughuli za mazishi, hatimaye, kuweza kubadilika na kuishi kulingana na matakwa ya jamii yao. Kimsingi, tija mojawapo ya fasihi inayotumika katika maombolezo ni kuleta mabadiliko chanya kulingana na misingi ya tamaduni inayozingatiwa (Mulokozi, 2003; M’Ngaruthi, 2008). Kwa kuongozwa na msingi wa Nadharia ya Sosholojia unaosisitiza kwamba upo uhusiano mkubwa kati ya fasihi na jamii; ni dhahiri kwamba mtani hubainisha yale yaliyopo na yanayotokea katika jamii yake kwa kutumia umbuji unaokidhi mahitaji ya uwasilishwaji wa maudhui yanayokusudiwa ili kuleta mabadiliko chanya.

Pamoja na vichekesho, umbuji wa watani katika maombolezo ya Wangoni hubainika kupitia malumbano yanayohusisha pande mbili. Malumbano ya watani ni mbinu ya kisanaa inayohusisha maneno ya kufanyia mzaha au dhihaka kwa kuelezana mwenendo au utaratibu wa maisha ya jamii (Simiyu, 2011). Malumbano hayo hufanywa kwa majibizano pasipo kuathiri azma ya ufikishaji wa maudhui kwa hadhira lengwa. Naye Kutwa (2021) anaeleza kwamba malumbano ya watani katika mazishi ya jamii ya Kiafrika, utendekaji wake hukitwa katika misingi ya kaida za jamii husika. Kwa Wangoni, imebainika kuwa malumbano wakati wa maombolezo mara nyingi hufanywa na watani wawili au zaidi wakivaa uhusika, mathalani, wa marehemu, jamii, kiongozi wa dini au wafiwa. Upande mmoja huwakilisha kundi lenye tabia zinazofaa na mwingine huwakilisha kundi lenye tabia zisizofaa kulingana na azma ya kufikisha ujumbe unaolengwa. Imebainika kuwa mhusika mwenye mwenendo na tabia nzuri uhusika wake hulenga kuonya na kukosoa upande wa pili wenye tabia zisizokubalika katika jamii yao. Aidha, matokeo yanaonesha kuwa katika malumbano hayo upande unaokosoa mara

nyingi hutumia lugha ya mafumbo yanayoambatana na kejeli katika kufikisha ujumbe husika huku upande mwingine ukijitetea. Hata hivyo, mwisho wa malumbano hayo upande unaoonywa hukubali upungufu wake na kukiri kubadilika kwa vitendo au lugha ya unyenyekevu. Malumbano yafuatayo ya watani X4 yanathibitisha hoja hii:

Mtani 1: *Bwelayi nikujobila ve mau.*

Tafsiri: Njoo nikuambie we mama.

Mtani 2: *Una kyani cha kunijovela nene. Hambayi kumadimba wenga.*

Tafsiri: Una jambo gani la kuniambia. Nenda zako bustanini wewe.

Mtani 1: *Mwimeka lenu gavili koki wenga. Mna cha kujova hinu?*

Tafsiri: Mnaringa leo yako wapi wewe. Mna cha kusema sasa?

Mtani 2: *Mbwelili mwavene. Tivakemalili lepi.*

Tafsiri: Mmekuja wenyewe. Hatujawaita.

Mtani 1: *Muweza kujizika? Lelu tivalekela malilu nginu*

Tafsiri: Mnaweza kujizika? Leo tunawaachia msiba wenu.

Mtani 2: *Lepa mlongo, pepayi mlongo tiweza lepi.*

Tafsiri: Hapana ndugu, tafadhali ndugu hatuwezi.

Mtani 1: *Kwa vayinu mbwitu kuhamba, mwajovayi mujizika mwavene?*

Tafsiri: Kwa wenzenu hampendi kushiriki, mlidhani mnajizika wenyewe?

Mtani 2: *Tipiliki mlongo pepayi tibudili.*

Tafsiri: Tumesikia ndugu yangu tafadhali tumekosa.

Mtani 1: *Mlolayi lelu mlolayi, vandu vahidi apa.*

Tafsiri: Tazameni leo watu wamekuja hapa

Mtani 2: *Ena ena tibudili tete.*

Tafsiri: Ndiyo, ndiyo tumekosa sisi.

**Chanzo:** Utafiti (2023)

Mtani 1 amevaa uhusika wa jamii na Mtani 2 amevaa uhusika wa wafiwa. Uwasilishaji wa maudhui kupitia malumbano haya unakwenda sambamba na vitendo mbalimbali. Kwa mfano, watani kuonesha vitu vilivyopo na watu waliokuja, kuruka, kulia, kucheka kwa kebehi na hata kutoa adhabu kwa mkosaji. Mathalani, katika kipengele cha Mtani 1 kisemacho: *Kwa vayinu mbwitu kuhamba, mwajovayi mujizika mwavene?*, chenye maana ya 'kwa wenzenu hampendi kushiriki, mlidhani mnajizika wenyewe?' Anapotamka fumbo hili hucheka na uso wake kuonesha kebehi kwa wafiwa huku akiwatazama na kuwanyoshea vidole walipoketi. Umbuji unaotumika kufikisha ujumbe huu unaleta tafakuri ya kina kwa watazamaji na wasikilizaji, hasa wafiwa. Mtani aliyevaa uhusika wa wafiwa jukumu lake ni kuomba msamaha kwa unyenyekevu kulingana na mila na desturi zao. Kwa mfano, kipengele cha Mtani 2 kisemacho: *Tipiliki mlongo pepayi tibudili* chenye maana ya 'tumekusikia ndugu yangu tafadhali tumekosa', anapotamka maneno hutenda vitendo mbalimbali. Mathalani, mhusika

anaweza kugaagaa chini au kumsogelea mtani anayelumbana naye na kumshika mkono ikiwa ni ishara ya kuomba msamaha kwa tabia iliyobainika kuwa ni kinyume na misingi ya utamaduni wao. Hufanya haya kwa niaba ya wafiwa na vitendo vyake huonesha kuwa amevaa uhusika wao. Matokeo yanaonesha kuwa kama mtani aliyevaa uhusika wa wafiwa amepewa adhabu inayohusisha kutoa kitu fulani kama vile kuku au fedha, huenda kwa wafiwa kuwataka watoe fedha hiyo kisha huikabidhi kwa mtani husika.

Vilevile, matokeo yanaonesha kuwa hakuna kupinga adhabu inayotolewa na mtani kama asemavyo msailiwa F: “Wanaopewa adhabu, kazi yao ni kutekeleza na kuomba msamaha kulingana na utamaduni wetu. Hivyo, hakuna kubishana na mtani, hasa wakati wa maombolezo”. Wangoni katika kuishi kwao, kubishana na mtani ni ukiukwaji wa maadili kama asemavyo Kenyatta (2004) kwamba katika jamii ya Wangoni, kuthamini mamlaka za kitamaduni, wakiwamo watani ni suala linalodhihirisha uzingatizi wa maadili katika jamii hiyo. Kwa hiyo, katika maombolezo yao, mtani hupewa thamani ya kusikilizwa na kujaliwa kwa kiwango kinachosawiri ukweli wa maisha yao.

Ufikishaji wa maudhui kwa malumbano husaidia ujumbe kufika vyema kwa hadhira lengwa kwa sababu hakuna anayeweza kukasirika kutokana na ukweli wa ujumbe unaotolewa na watani hao. Zaidi, malumbano hayo huwafanya walengwa waweze kutafakari juu ya tabia waliyo nayo. Kwa kujiegemeza katika msingi wa Nadharia ya Sosholojia ya Kifasihi unaodai kuwa upo uhusiano mkubwa kati ya fasihi na jamii, ni wazi kuwa umbuji wa watani huakisi utamaduni wa jamii hiyo. Matokeo yanaonesha kuwa wakati wa maombolezo vionjo vinavyoingizwa katika malumbano ya watani hutegemea hali na nafasi za wafiwa pasipo kuathiri ukweli wa maisha na ushiriki wao katika shughuli za mazishi. Licha ya kuwalenga wafiwa, ujumbe huo huwafundisha na kuwaonya wengine wenye tabia kama hizo ili watambue kuwa kushiriki katika shughuli zinazohusiana na suala la kifo ni lazima kwa mujibu wa tamaduni za jamii ya Wangoni. Sambamba na nukuu hiyo msailiwa G anabainisha vyema jambo hili kwa kusema:

Katika jamii yetu suala muhimu sana kushiriki ni mazishi. Kuna wengine wanajiona wanakosa muda wa kufanya hivyo. Jamii inawaangalia tu. Siku wakipata msiba nyumbani mwao, watani kama wawakilishi wa jamii katika kufikisha hisia zao, tunawaambia ukweli bila soni. Mara nyingi tunaigiza matendo yao au ya marehemu ili kutoa funzo lenye nia ya kukosoa mwenendo huo mbaya. Na, tunapogusa tu suala kama hilo, utaona watu waliopo wanaitikia kwa nguvu na kwa hisia kali, na wakati mwingine hutushangilia kwa makofi. Hii inamaanisha kwamba, ni tabia ambayo jamii nzima haifurahishwi nayo. Kimsingi, kueleza ukweli ni moja ya jukumu letu sisi watani tulioaminiwa na familia au ukoo husika. Kwa hiyo, tunapoigiza tunaweka *manjonjo* (madoido) na mbwembwe nyingi kiasi kwamba unaweza usichoke kutusikiliza. Pia, tunachopeka lugha ya kejeli ili kuleta uzito wa ujumbe unaowasilishwa. Uchopekaji huo huakisi

ufundi fulani wa kuigiza kwa mafumbo kwa namna isiyoathiri mila na desturi zetu.

**Chanzo:** Utafiti (2023)

Nukuu hii inathibitisha kuwa maudhui yanayowasilishwa na watani wakati wa maombolezo hulenga zaidi kubainisha ukweli wa tabia miongoni mwa wanajamii, hususani wafiwa. Matokeo yanaonesha kuwa wakati wa malumbano ya watani, waombolezaji hutambua jukumu lao na kuwapa nafasi ya kuwatazama na kusikiliza kinachowasilishwa kwa makini. Kwa hiyo, umahiri unaobainika kupitia uigizaji wa watani wenye kutawaliwa na vitendo, lugha ya kebehi na sauti yenye madoido huibua hisia za tafakuri kwa wafiwa na kujifunza namna jamii yao inavyowatazama. Hivyo, kuchukua hatua za kubadili mwenendo na tabia yao. Aidha, maigizo ya watani huwakumbusha wanajamii wengine kwamba, suala la huzuni linapaswa kuthaminiwa na kila mmoja wapo katika jamii na hivyo, ushirikiano katika jambo hilo ni muhimu sana. Haya yanabainishwa vyema na Ponera na Duwe (2018) kwamba katika jamii ya Wangoni umoja na mshikamano ni nguzo muhimu katika kuyaendea masuala mbalimbali ya kijamii, yakiwamo yanayohusiana na suala la kifo.

### **4.3 Mbolezi**

Mbolezi ni nyimbo za maombolezo katika jamii nyingi za Waafrika, ambapo uimbaji wake kufungamanishwa na utamaduni wa jamii husika (Mlaga, 2017). Utamaduni huo unaweza kufanana au kutofautiana kutoka jamii moja na nyingine katika muktadha wa utendaji na matumizi ya lugha. Mbolezi zinapoimbwa huwasilisha maudhui yanayoisawiri jamii husika kama vile: kumwomba marehemu kwa Mungu, kutoa wasifu wake, kuagana naye na kuonesha kuwa bado wanampenda mpendwa wao (Okpewho, 1992). Kwa mujibu wa makala hii, mbolezi za Wangoni hurejelea nyimbo za maombolezo zinazoimbwa katika mazingira yao kwa kusawiri utamaduni wao halisi. Kwa hiyo, mbolezi zinazoimbwa nje na mazingira yao halisi, hazikuhusishwa katika uchunguzi. Hii ni kutokana na mawanda ya utafiti ambayo yalijikita katika kuchunguza mbolezi zinazoimbwa katika mazingira halisi ili kubaini uhalisi wa umbuji wa watani kupitia mbolezi hizo. Kulingana na utamaduni wao, mbolezi huimbwa na jamii nzima wakati wa kuomboleza (Duwe, 2022). Hata hivyo, mtani au kikundi cha watani wanapokuwa na lengo la kufikisha ujumbe fulani kwa wafiwa au jamii, hutumia mbolezi kwa ufundi unaokidhi azma ya utani wao. Mbolezi hizo zinaweza kuwa za kukejeli, kusifu au kuonya wafiwa au jamii kulingana na ulazima wa uwasilishaji wa maudhui husika. Imebainika kwamba mtani anaweza kutumia mbolezi zile zinazotumika katika maombolezo yao au huimba nyingine kwa kuweka vionjo vya maneno husika kulingana na maudhui yanayolengwa kufikishwa kwa hadhira.

Imebainika kuwa uimbaji wa watani katika maombolezo ya Wangoni kupitia mbolezi hutawaliwa na vionjo vyenye hisia ya shangwe na matumizi ya lugha ya kejeli. Kimsingi, hisia za shangwe katika maombolezo ya Wangoni hubainika kupitia vitendo vya watani kama vile upigaji wa makofi na vigelegele vinayokwenda sambamba na uwasilishaji wa maudhui lengwa. Watani wanaweza kuimba nyimbo zinazotumika na kuzoeleka katika jamii yao ila huweka msamiati mwingine kulingana na maudhui lengwa. Pia, wanaweza kuimba wimbo usiojulikana kwa waombolezaji. Hata hivyo, hadhira inampa nafasi ya kumtazama na kusikiliza ujumbe uliomo katika mbolezi inayoimbwa. Kwa mfano, mtani X5 anaimba mbolezi hii:

*Mjiyingayi mwenga tete tivili apa pamongo, ndila ya tawoha mwenga,  
Tibwelili tete tibwelili apa. Tina mahengu ga kukita tigalekili tibwelili  
apa,  
Mwavene lelu mwanja muktikiki apa? Tete tiwuka lepi lelu apa,  
Tivemba tawoa lelu apa, mwenga mwenga mlolayi lelu apa,  
Mavembu ga mmonga avile lepa lelu apa, mlolayi kwa vayinu lelu  
gavili apa,  
Lelu swiswiswi apa, mjovai mwa vabwina kwa vandu lelu apa,  
Mchikolili lelu nu apa, leka pavinayi lelu muvili jiiii apa (x2).*

**Tafsiri:**

Jamani mjikubali tu sasa na sisi tupo pamoja nanyi, hii njia ya sisi sote,  
Tumekuja sisi tumekuja hapa, tuna kazi za kufanya lakini tumeziacha  
na kuja hapa,  
Wenyewe leo mngefanyaje hapa? Sisi hatutoki hapa leo,  
Tunalia sote hapa leo, jamani jamani mtazame kwa wenzenu leo yapo  
hapa,  
Leo mpo kimyakimya hapa, utadhani ni wema sana kwa wengine,  
Mmechoka leo mpo kimya, wacha pawauume leo mpo kimya (x2).

**Chanzo:** Utafiti (2023).

Umbuji katika uimbaji wa mbolezi hii umetawaliwa na lugha ya masimango na vitendo kama vile kuwanyoshea vidole wafiwa na kupiga makofi, kucheza na hata kulia. Umbuji huu huifanya hadhira itulie na kusikiliza kwa makini kinachoimbwa. Imebainika kwamba idadi ya beti za wimbo inategemeana na utoshelevu wa maudhui lengwa. Kwa mantiki hiyo, mtani anaweza kuimba ubeti mmoja au mbili na kurudia mara mbili au zaidi ili ujumbe unaolengwa ufike vyema kwa hadhira yake. Maudhui yanayobainika hapa yanalenga kuwafariji na kuonesha hisia za jamii kuhusu mwenendo usioridhisha unaofanywa na wafiwa. Kwa mfano, mstari usemao, *Lelu swiswiswi apa, mjovai mwa vabwina kwa vandu lelu apa*, wenye maana ya ‘leo mpo kimya hapa, utadhani ni wema sana kwa wengine’, huimbwa kwa lugha yenye mkazo unaoashiria kuwakejeli wafiwa. Vilevile, imebainika kwamba wakati wa utendekaji, mtani hushangiliwa na waombolezaji wengine kwa

kuwa anachokiwasilisha kinaakisi hisia za jamii nzima. Sambamba na wimbo huo, msailiwa H anashadidia:

Kuimba katika jamii yetu ni asili ambapo tumerithi tangu enzi za babu zetu. Katika jamii yetu, tunatumia sana nyimbo wakati wa maombolezo ili kutoa ujumbe kwa walengwa. Wimbo unaweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watu. Namna ya upachikaji wa vionjo hutegemeana na kusudi la wimbo huo. Panapotokea maombolezo katika jamii yetu nyimbo huweza kuimbwa na jamii nzima wakiongozwa na kikundi cha uimbaji. Hata hivyo, mtani anaweza kutumia nyimbo zilezile ila anabadilisha maneno kuendana na kile anacholenga kuwasilisha kwa hadhira yake. Hadhira inapona mtani anaimba kwa sauti wimbo fulani inatulia na kumsikiliza kwa makini kwa kuwa inajua kwamba ana jambo la muhimu kwao. Uimbaji wake huwa tofauti kidogo na unaoanzishwa na wanakikundi waliozoeleka katika jamii yetu. Yeye hafuati misingi ya uimbaji wa wimbo husika. Mara nyingi uimbaji wake huambatana na vitendo kama vile kulia, kuhuzunika au kucheka ikiwa ni ishara ya kuwakebehi wafiwa.

**Chanzo:** Utafiti (2023).

Nukuu hii inathibitisha kuwa umbuji wa watani kupitia mbolezi hubadilika kulingana na kusudi la kuwasilisha maudhui lengwa. Kwa hiyo, hakuna mtiririko mmoja unaozingatiwa na watani katika uimbaji wao. Kwa ujumla, matokeo yanaonesha kuwa hisia za shangwe hutawala wakati wa uimbaji huo. Kwa kuzingatia mtazamo wa wanasosholojia wa kifasihi kwamba kuna uhusiano mkubwa baina ya fasihi na jamii, uwasilishaji wa maudhui kupitia umbuji wa watani katika maombolezo ya Wangoni huakisi kaida za jamii hiyo. Kwa hiyo, mtani huimba wimbo kulingana na uhusiano wake wa kimaudhui yanayolengwa kuwasilishwa. Kwa ujumla, Wangoni tangu walipoingia katika eneo la Tanzania, hususani mkoa wa Ruvuma walikuwa wanaimba nyimbo mbalimbali, zikiwamo mbolezi zilizoakisi utamaduni kwenye masuala ya lugha hadi utendekaji wake (Ebner, 2009). Hadi sasa jamii hiyo inaendelea kutumia nyimbo kama nguzo muhimu katika kuwasilisha maudhui lengwa kwa hadhira kwa kutumia umbuji unaoakisi utamaduni wao halisi (Duwe, 2022). Hivyo, katika matukio mbalimbali ya kijamii, ikiwamo mazishi yao, watani hutumia pia mbolezi ili kufikisha ujumbe unaolengwa kwa hadhira.

## **5.0 Hitimisho**

Makala hii imejadili kuhusu umbuji wa watani katika maombolezo ya Wangoni. Mjadala umetokana na data zilizopatikana uwandani kupitia mbinu ya usaili na ushuhudiaji wa matukio kadhaa yaliyoambatana na maombolezo. Mjadala umedhihirisha kwamba kwa Wangoni umbuji wa watani katika maombolezo yao hujipambanua kupitia maigizo, nyimbo na semi. Vipengele hivyo huongozwa na

uzingatiaji wa misingi ya mila na desturi husika katika muktadha wa vitendo vinavyokamilisha umbuji huo. Vitendo hivyo huambatana na matumizi ya lugha ya kejeli au masimango na mafumbo. Madhumuni ya kutumia umbuji huo katika maombolezo yao ni: kwanza, kuwasahaulisha wafiwa kama wapo katika huzuni. Hii ni kutokana na ustadi wao wa kuwasilisha maudhui yanayobebwa katika nyimbo, maigizo au semi hizo. Hivyo, wafiwa hufurahi na kulichukulia jambo hilo kama la kawaida kutokana na ukweli kwamba, huzuni ikizidi huweza kusababisha madhara ya kiafya kwa wahusika. Kwa msingi huo, hata maudhui yale yenye kuibua hisia za huzuni, hasa yanayodokeza kuwapo kwa upweke kwa wafiwa, huchukuliwa na hupokelewa kwa kiwango kisicholeta huzuni kubwa kwao. Pili, ufundi wa kuwasilisha maudhui unaotumiwa na watani huifanya hadhira isichoke kusikiliza au kutazama kinachotendwa pasipo hadhira kushikwa na chukizo lolote. Tatu, umbuji huo hulenga kuenzi na kuendeleza utamaduni wa kutaniana kama nguzo muhimu ya kuwasilisha maudhui kwa hadhira.

### Marejeleo

- Coser, L. (1972). *Sociology through Literature: An Introductory Reader*. The University of California: Prentice-Hall.
- Duwe, M. (2022). *Uchimuzi wa Eskatolojia ya Waafrika katika Mbolezi za Wangoni*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Ebner, P.E. (2009). *The History of the Wangoni*. Songea: Peramiho Printing Press.
- Glicksberg, C. I. (1972). *Literature and Society*. The Hague: Martinus Nijhoff.
- Kenyatta, P.A. (2004). *Imani ya Wamatengo Juu ya Uchawi, Kifo, Kindorobo na Uganga wa Kienyeji*. Songea: Peramiho Printing Press.
- Kirumbi, P.S. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.
- Khosa-Nkatini, H.P. (2022). "Patriarchal Nature of Mourning from an African Perspective". *HTS Teologiese Studies/Theological Studies*. 78(2): 1-7. Inapatikana katika <https://www.ajol.info/index.php/hts/article/view/248168>. Ilisomwa tarehe 24 Aprili 2024.
- Kutwa, H.A. (2021). *Ujumi katika Malumbano ya Watani: Mifano kutoka Familia za Wadigo, Tanga Mjini*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mauya, A.B. (2006). *Semi, Maana na Matumizi*. Dar es Salaam: TUKI.
- Migodela, W. (2019). "Uainishaji wa Nyimbo za Tiba Asili". *TALUFAKITA*. (1): 65-78.
- Miruka, O. (2005). *Incounter with Oral Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mlaga, W.K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi: Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers.



- M'Ngaruthi, T.K. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mrikaria, S.E. (2010). "Kejeli na Fasihi ya Kiswahili Tanzania". *Swahili Forum*. 17(1): 104-125.
- Mulokozi, M.M. (2003). "Utafiti wa Fasihi Simulizi". *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. 3(1): 1-25.
- Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Mzandi, M. (2011). *Nafasi ya Utani Msibani na Harusini kwa Kabila la Wadigo*. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Ngonyani, D.S. (1988). *A Comparative Study of Kindendeule, Kingoni and Kimatengo*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character, and Continuity*. Bloomington: Indiana University Press.
- Ponera, A.S. na Duwe, M. (2018). "Vijenzi vya Falsafa ya Uduara katika Sanaa za Maonesho za Jamii ya Wangoni". *Mwanga wa Lugha*. 2(1): 1-13.
- Simiyu, W.F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Bookshop.
- Simiyu, W.F. (2015). *Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- TIE. (2019). *History for Secondary Schools: Students Book Form Two*. Dar es Salaam: TIE.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.
- Wasamba, P. (2015). *Contemporary Oral Literature Fieldwork*. Nairobi: University of Nairobi.